OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
MTIHANI WA UTAMIRIFU KIDATO CHA NNE
MKOA WA ARUSHA
KISWAHILI

MSIMBO NA. 021
MUDA: SAA 3:00 MEI: 2025

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu A, B na C zenye jumla ya maswali kumi na moja (11)
2. Jibu maswali yote katika sehemu A and B na maswali mawili (02) kutoka sehemu C ambapo swali la tisa (09) ni la lazima.
3. Shemu 'A' in alama kumi na sita (16), sehemu 'B' ina alama hamsini nan ne (54) na sehemu 'C' in alama thelathini (30)
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali.
5. Majibu yote yaandikwe kwa kalamu yenye wino wa blue au mweusi.
6. Vifaa vya mawasiliano na vitu visivyoruhusiwa havitakiwi katika chumba cha mtihani
7. Andika namba yako ya mtihani katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

SEHEMU A (Alama 16)
Jibu maswali yote katika sehemu hii

1. Katika kipengele (i) – (x) chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika kijitabu cha kujibia.

i) Uwasilishaji wa kazi ya fasihi unaotofautiana kati ya mtunzi mmoja na mwingine huitwa
A. Mtindo B. Muundo C. Wahusika
D. Fani E. Maudhui

ii) Mzee Kuomba ana watoto watano, wanne wamebatizwa jina kutoka kwenye nomino pekee na mmoja amebatizwa jina kutoka nomino dhahania. Je! Unafikiri mtoto wa mzee Kuomba ambaye ana jila la nomino dhahania atakuwa nani kati ya hawa?
A. Januari B. Faraja C. John D. Asha E. Masanja

iii) 'Mtangazaji wa Televisheni huhakikisha watazamaji wanapata habari sahihi na kwa wakati'. Katika fasihi kazi hiyo hufanywa na nani kati ya hawa wafuatao?
A. Wasikilizaji B. Hadhira C. Wasomaji D. Wasomi E. Fanani

iv) Mzizi wa neno 'kula' ni:-
A. -la- B. -l- C. -kul- D. -ul- E. kula

v) Neno 'chawa' lenye maana ya mfuasi au kibaraka wa mtu fulani linaweza kuingizwa kwenye kundi gani la msimu kati ya hii?
A. Misimu ya kipekee B. Misimu ya kihuni
C. Misimu ya kitarafa D. Misimu Zagao E. Misimu Binafsi

vi) Ni mambo gani muhimu ya kuzingatia katika kuteua maneno na miundo ya tungo wakati wa mazungumzo?
A. Mada, Muktadha na mazungumzo ya ana kwa ana
B. Mada, msikilizaji, mzungumzaji na njia ya mawasiliano
C. Mada, muktadha, lengo na uhusiano wa wazungumzaji
D. Mada, mazungumzo na uhusiano wa mazungumzo
E. Mada, muziki, utoshelevu na uhusiano wa mazungumzo

vii) Hoja za msingi zinazotetea kuwa Kiswahili asili yake ni Kiarabu imeegemea katika:-
A. Biashara ya utumwa B. Dini ya Kiislamu C. Msamiati
D. Waarabu kuwa Waafrika E. Lugha za kibantu

viii) Ipi ni tofauti ya msingi kati ya mashairi na ngonjera?
A. Mpangilio wa vina na mizani
B. Idadi ya mizani na mishororo
C. Majibizano baina ya watu wawili au zaidi
D. Mpangilio wa silabi na lugha ya mkato
E. Mapigo ya kimziki na ridhimu

ix) Tamthiliya ambayo mwishoni wahusika wake wakuu huonesha kufanikiwa inaitwa:-
A. Tanzia B. Ramsa C. Futuhi D. Ngoswe E. Kiliochetu

x) Mkuu wa shule aliwashauri wanafunzi waliofanya vibaya kwenye mtihani wa Kiswahili kwa kuwaambia "Kazeni Kamba". Je! Mkuu wa shule alitumia kipera gani kwa kuwasihi wanafunzi?
A. Nahau B. Methali C. Kitendawili D. Fumbo E. Msemo

2. Oanisha maelezo yaliyoko fungu 'A' na dhana zilizoko fungu 'B' kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kukamilisha maana.

| FUNGU A | FUNGU B |
|---|---|
| i) Kisiu | A. Huzungumzwa Kisiwa cha Pate |
| ii) Kiamu | B. Huzungumzwa Kisiwa cha Lamu Kaskazini |
| iii) Kimwani | C. Huzungumzwa Mombasa |
| iv) Kipemba | D. Huzungumzwa jimbo la shaba Zaire |
| v) Kirumba (kiranga) | E. Huzungumzwa Kaskazini mwa Msumbiji |
| vi) Kimgao | F. Huzungumzwa Pwani ya Kusini mwa Tanzania |
| | G. Huzungumzwa kisiwa cha Pemba |
| | H. Huzungumzwa mpakani mwa Kenya |
| | I. Huzungumzwa Tanga. |

3. a) Eleza maana ya mofu
   b) Bainisha Mofu nne (04) za kauli ya kutendeka kisha tunga sentensi moja kwa kila mofu huku ukipigia mstari mofu hiyo.

4. a) "Chakubanga" ni mwanafunzi wa kidato cha nne (iv) katika shule ya sekondari Ujamaa. Alipokuwa njiani alikutana na rafiki yake "Mapito" anayesoma shule ya Jirani hajui umuhimu wa kuunda maneno mapya katika lugha. Je, unafikiri "Chakubanga" alimwelezaje rafiki yake? Toa hoja nne (4).

   b) Njia zipi zimetumika kuunda maneno yafuatayo?
      i) TAKILUKI
      ii) Chajio
      iii) Mwanajeshi

5. a) Kishazi ni tungo ambayo inaweza kutoa taarifa kamili au isiyokamili. Fafanua aina kuu mbili za kishazi tegemezi.

   b) Changua sentensi ifuatayo kwa kutumia mkabala wa "kidhima" njia ya matawi sentensi: "Nitakuja kesho asubuhi"

6. "Msigiri" alimwambia "Msiriri" kuwa Kiswahili ni Kibantu. "Msiriri" alibisha na kudai kuwa Kiswahili ni Kiarabu. Ungana na "Msigiri" kutetea hoja yake kwa kutumia msamiati kwa kutoa mifano miwili (02), muundo wa sentensi mifano miwili (02).

7. Miongoni mwa mambo yaliyojadiliwa katika Riwaya ya "Joka la Mdimu" ni matatizo sugu yaliyopo katika jamii yetu. Fafanua matatizo hayo kwa kutoa hoja sita (6).

8. Andika kumbukumbu za kikao cha wanafunzi kuhusu sherehe ya kumuaga Mkuu wao wa shule aliyepata wadhifa wa kuwa Afisa Elimu Mkoa. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe nane (8) tu.

## SEHEMU C: (ALAMA 30)

Jibu maswali mawili kutoka sehemu hii.
Swali la 9 ni la lazima na kila swali lina alama 15.

## ORODHA YA VITABU

*USHAIRI*

| | | |
|---|---|---|
| - *WASAKATONGE* | - | *M.S Khatibu (OUP)* |
| - *MALENGA WAPYA* | - | *TAKILUKI (DUP)* |
| - *MASHAIRI YA CHEKACHEKA* | - | *T.A. Mvungi (EP & D. LTD)* |

*RIWAYA*

| | | |
|---|---|---|
| - *TAKADINI* | - | *Ben J. Hanson (MBs)* |
| - *WATOTO WA MAMANTILIE* | - | - *E. Mbogo (H. P)* |
| - *JOKA LA MDIMU* | - | *A. J. Safari (H. P)* |

*TAMTHILIYA*

| | |
|---|---|
| - *NGOSWE PENZI KITOVU CHA UZEMBE* | - *E. Semzaba (Esc)* |
| - *ORODHA* | - *STEVE REYNOLDS (MA)* |
| - *KILIO CHETU* | - *MEDICAL AID FOUNDATION* |

9. Washairi wengi ni wataalamu wazuri waliobobea katika kutumia "jazanda" katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Tumia "Jazanda" tatu kwa kila diwani katika diwani mbili ulizosoma darasani kuthibitisha kauli hiyo.

10. Lugha anayoitumia mwandishi katika kazi ya fasihi ndiyo inayosaidia katika kufikisha ujumbe kwa hadhira yake. Kwa kutumia riwaya teule mbili (02) ulizosoma. Jadili jinsi wasanii wa riwaya hizo walivyotumia kipengele cha tamathali za semi.

11. Waandishi wengi huandika kazi zao kwa lengo la kutoa funzo kwa jamii anayoiandikia. Kwa kutumia tamthiliya mbili (02) zilizoorodheshwa thibitisha ukweli wa kauli hii.

ushahidi wa mariko polo
ushahidi wa Alli idris
ushahidi wa alli masudi

malenga
ulimi
usiropokropoke, ouyu
ewe ulimi sikia

Ua
ua limesituliza, mtini langningia
Mwanyewa lanitunza, furahani [illegible]
Rangi yako yalikisanifu, moyoni laningoa
Samaki mtungoni
watu wanaokandamizwa [illegible]

Wasaka
Taswira Jiko la shamba
Taswira ya [illegible]

uongozi mbaya
wanapigana
wanaumizana
wanauwana
kisa fungo la ugali

[illegible] Jiko la shamba, [illegible]
[illegible]
[illegible]